# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 034 OKTOBA 2023

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY



1 TMA YATOA RASMI UTABIRI WA MVUA MAENEO YANAYOPATA MSIMU MMOJA KWA MWAKA

2 DKT. CHANG'A AFANYA KIKAO NA MKURUGENZI WA SHIRIKA LA HALI YA HEWA DUNIANI (WMO) OFISI YA KANDA YA AFRIKA, DKT. AGNES KIJAZI KUJADILI VIPAUMBELE VYA TMA




3 FAHAMU ZAIDI:
HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI NOVEMBA, 2023



## KITAIFA

# TMA YATOA RASMI UTABIRI WA MVUA MAENEO YANAYOPATA MSIMU MMOJA KWA MWAKA

**Dar es Salaam**




Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilitoa rasmi mwelekeo wa mvua za Msimu kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka ambayo ni mikoa ya Tabora, Katavi, Kigoma, Singida, Dodoma, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, Lindi, Mtwara, Ruvuma na Kusini mwa Morogoro. Taarifa hiyo ilisema kipindi cha nusu ya msimu (Novemba 2023 hadi Januari, 2024) kinatarajiwa kuwa na mvua nyingi ukilinganisha na nusu ya pili (Februari hadi Aprili 2024), uwepo wa El-Niño unatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika mvua za Msimu.

"Mvua za Juu ya Wastani hadi Wastani zinatarajiwa katika maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro, mikoa ya Iringa, Lindi, Mtwara, Singida, Dodoma, kaskazini mwa

mkoa wa Katavi, Kigoma na Tabora. Aidha, mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa kusini mwa mkoa wa Katavi, mikoa ya Njombe, Rukwa, Songwe, Mbeya na Ruvuma". Alisema Dkt. Ladislaus Chang'a, Kaimu Mkurugenzi Mkuu TMA na Makamu Mwenyekiti Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabiachi (IPCC) wakati wa mkutano na vyombo vya habari kuhusiana na mwelekeo wa mvua za Msimu, katika ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam,Tarehe 31 Oktoba, 2023.

Dkt. Chang'a alibainisha athari zinazoweza kujitokeza ikiwa ni vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri ukuaji wa mazao na miundombinu ya kilimo, vile vile, kina cha maji katika mito na mabwawa kinatarajiwa kuongezeka, aidha, Dkt. Chang'a alitoa ushauri kwa wadau mbalimbali kuzingatia matumizi endelevu ya uhifadhi wa rasimali maji.

Katika hatua nyingine, Dkt. Chang'a alifafanua kuwa Msimu wa Vuli kwa miezi ya Oktoba hadi Disemba, 2023 katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, Pwani (ikijumuisha kisiwa cha Mafia) pamoja na Zanzibar (visiwa vya Unguja na Pemba) utabiri wake ulitolewa tarehe 24 Agosti, 2023.



## KIMATAIFA

# DKT. CHANG'A AFANYA KIKAO NA MKURUGENZI WA SHIRIKA LA HALI YA HEWA DUNIANI (WMO) OFISI YA KANDA YA AFRIKA, DKT. AGNES KIJAZI KUJADILI VIPAUMBELE VYA TMA

**Dodoma**




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi, "Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC)", Dkt. Ladislaus Chang'a, alifanya kikao na Mkurugenzi wa WMO Ofisi ya Kanda ya Afrika (WMO Regional Office for Africa – RAF), Dkt. Agnes Kijazi kujadili vipaumbele vya Taasisi za Hali ya Hewa Barani Afrika ikiwa ni pamoja na TMA. Majadiliano hayo yalifanyika kwa njia ya mtandao na kuhudhuriwa na baadhi ya watumishi wa TMA na WMO Ofisi ya Kanda ya Afrika iliyopo Addis Ababa, Ethiopia.

Wakati akitoa neno la ufunguzi wa majadiliano hayo, Dkt. Agnes Kijazi alisema kikao hicho ni mwendelezo wa vikao ambavyo amekuwa akivifanya na Wakuu wa Taasisi za Hali ya Hewa za nchi za Afrika, ambapo alisema lengo la vikao hivyo ni kufahamu changamoto zinazozikabili Taasisi za hali ya hewa katika Bara la Afrika, na vipaumbele katika kuzitatua changamoto hizo.

Dkt. Chang'a alimshukuru Dkt. Kijazi kwa kikao na kumpongeza kwa utaratibu mzuri wa kukutana na Taasisi za hali ya hewa, jambo ambalo litasaidia kutatua changamoto zinazokabili nchi nyingi za Bara la Afrika katika utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa jamii. Dkt. Chang'a alifafanua kwamba kipaumbele kikuu cha TMA ni kutoa huduma

bora za hali ya hewa zinazokidhi mahitaji ya watumiaji wote, ambazo pia zitachangia ipasavyo katika mkakati wa Umoja wa Mataifa wa "Tahadhari za mapema kwa wote (**Early Warning for All – EW4All)**". Alisema kwa upande wa Tanzania, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kushirikiana na kusaidia Mamlaka katika kuboresha utoaji wa huduma za hali ya hewa, ikiwa ni pamoja na kuwekeza katika miundombinu ya uangazi na uchakataji wa taarifa na kufadhili mafunzo kwa wataalamu. Sambamba na jitihada zinazofanywa na Serikali Dkt. Chang'a alisema, bado kuna changamoto katika kukidhi mahitaji ya watumiaji.

Alitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni: mtandao wa vituo vya uangazi wa hali ya hewa usiotosheleza; miundombinu isiyotosheleza ya kuchakata data na utabiri wa hali ya hewa, kuandaa taarifa mahsusi za kila kundi la watumiaji; njia rafiki zenye ufanisi na zenye gharama nafuu za kuwafikishia taarifa watumiaji walio katika mazingira magumu au vijijini ambao hawana simu au wasiotumia mitandao ya kijamii; hitaji la kuongeza ujuzi wa wataalamu kuendana na kasi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia; mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi.

Licha ya changamoto hizo, Dkt. Chang'a alifafanua maeneo ambayo TMA imepiga hatua na Itakuwa tayari kushirikiana na Taasisi za Hali ya Hewa za nchi nyingine za hali ya hewa barani Afrika. Alitaja maeneo hayo kuwa ni pamoja na matumizi ya mifumo ya ubadilishanaji wa taarifa na mawasiliano ya taarifa za hali ya hewa iliyobuniwa na wataalamu wa TMA ambayo imechangia kuboresha huduma za hali ya hewa nchini. Mifumo hiyo ni **"Digital Meteorological Observatory (DMO)", "Meteorological Aviation Information System (MAIS)", na "Marine Meteorological Information System (MMIS)"**. Maeneo mengine aliyotaja ambayo TMA imepiga hatua ni Huduma za Hali ya Hewa katika Usafiri na Usalama wa Anga, Utabiri wa hali ya hewa kwa njia ya mahesabu (Numerical Weather Prediction - NWP) na uangazi kwa kutumia teknolojia ya RADAR, ambapo mafunzo ya muda mfupi ya matumizi ya RADAR za hali ya hewa kwa wataalamu wa Taasisi za hali ya hewa za nchi za Afrika Mashariki yanatarajiwa kufanyika mwakani kwa uratibu wa TMA/NMTC na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO).

Kwa upande wake Dkt. Kijazi alimpongeza Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA kwa mafanikio ambayo TMA imepata na kusema kwamba maeneo ambayo TMA imepiga hatua yataweza kuzisaidia Taasisi nyingine za Hali ya Hewa za Bara la Afrika zinazohitaji ujuzi huo. Aidha, Dkt. Kijazi alipongeza kwa ushirikiano na mahusiano ya karibu kati ya TMA na Wizara na Taasisi nyingine za Serikali, jambo ambalo alisisitiza ni chachu katika kutatua changamoto nyingi zinazoikabili sekta ya hali ya hewa, hususan katika bara la Afrika. Aliongeza kuwa ni muhimu mahusiano hayo yakaendelea kuimarika. Kwa upande wa changamoto zilizowasilishwa, alisema ofisi yake itafanya majumuisho na kuandaa mpango wa kuzitafutia ufumbuzi. Katika hilo alishauri pia TMA kuzijumuisha changamoto katika mpango mkakati na kuendelea kushirikisha Serikali kwani Serikali ni mdau muhimu katika maendeleo ya sekta ya hali ya hewa.

JARIDA LA MWEZI

06 TOLEO NA. 034 OKTOBA 2023

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# FAHAMU ZAIDI

## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2023

Katika kipindi cha mwezi Novemba 2023, mvua za Msimu, 2023/2024 zinatarajiwa kuanza katika maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka. Katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka mvua zinatarajiwa kuendelea. Hata hivyo, ongezeko la mvua linatarajiwa nchini. Kwa upande mwingine, hali ya joto kiasi inatarajiwa kuendelea hususan katika baadhi ya maeneo yanayotarajiwa kupata vipindi vichache vya mvua.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| **Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):** | ♦ Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| **Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):** | ♦ Katika kipindi hiki, vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa kati wiki ya kwanza na ya pili.** |
| **Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):** | ♦ Vipindi vya mvua vinavyoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.** |
| **Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** | ♦ Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha mwezi Novemba,2023. **Aidha ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya kwanza na ya pili.** |
| **Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya pili na ya tatu ya mwezi.** |
| **Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):** | ♦ Vipindi vya mvua vinavyoambatana na ngurumo kwa baadhi ya nyakati vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa wiki ya pili na ya tatu.** |
| **Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** | ♦ Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya pili na ya tatu ya mwezi.** |
| **Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma):** | ♦ Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. **Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya tatu ya mwezi.** |

JARIDA LA MWEZI

07 TOLEO NA. 034 OKTOBA 2023

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# BIDHAA NA HUDUMA ZA TMA

## HUDUMA ZA HALI YA HEWA KWA SEKTA YA RASILIMALI MAJI

Mamlaka ya Hali ya hewa Tanzania inatoa huduma za hali ya hewa zinazosaidia sekta ya Rasilimali maji kudhibiti athari zinazohusiana na hali mbaya ya hewa. Huduma hizi zinatolewa kwa kufuata na kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Mamlaka inatoa huduma zifuatazo za hali ya hewa kwa shughuli za rasilimali maji**

(a) Taarifa za hali ya hewa za klimatolojia kama vile mvua, mvukizo na joto.
(b) Uvunaji wa maji ya mvua na miundombinu ya rasilimali maji.
(c) Utabiri wa mafuriko ukiwemo mwongozo.
(d) Mpango wa umwagiliaji.
(e) Mwelekeo wa msimu na taarifa huishwa za hali ya hewa.

**Wateja wa rasilimali maji hutumia huduma za hali ya hewa katika shughuli zifuatazo-**

(a) Shughuli za haidrolojia
(b) Usimamizi wa mabwawa
(c) Upangaji na usimamizi madhubuti wa rasilimali maji na Mabonde.
(d) Usimamizi wa mafuriko.








**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Monica Mutoni
Wilbert Muruke

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa

www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

TMAonline TV

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.